Haliuzwi

NOVEMBA 3, 2024

/islam-

IMAAN

Jamada I 1 1446

ISSN 5618 - NO. 504

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Kanda ya ziwa kicheko, meli mpya 2025

MIAKA MINNE MADARAKANI

Rekodi za Rais Mwinyi zambeba

Rais Mwinyi, ambaye aliingia madarakani akijipambanua kujikita katika sera ya uchumi wa buluu na kuunda wizara maalumu itakayosimamia eneo hilo, amepata mafanikio katika karibu kila sekta

> “Wengi walidhani hatutaweza, lakini haya tunayofanya ni salamu tosha, tumeahidi tumetekeleza na tutaendelea kutekeleza mengi bado yanakuja
>
> Rais wa Zanzibar, Dkt Hussein Mwinyi

Maadui wa mafanikio wanaishi ndani yetu

Mkutano nchi za Kiislamu kuleta nusra Palestina au siasa tu?

Shule za Imaan ufaulu juu darasa la saba

Ufaulu la 7 uwe chachu ya kufanya vizuri sekondari

Israel yatia fora kwa kuwa na kesi nyingi ICJ

Trump au Harris? Waislamu Marekani katika chaguo gumu

Mashirika ya kibinadamu yazidi kuwapambania Warohingya

Minne madarakani, rekodi za Rais Mwinyi zambeba

Adai mengi bado yanakuja

Wakati akitimiza miaka minne ya utawala wake, Rais wa Zanzibar, Dkt Hussein Mwinyi, ametajwa kama mmoja wa marais waliopata mafanikio makubwa zaidi visiwani humo.

Rais Mwinyi, ambaye aliingia madarakani akijipambanua kujikita katika sera ya uchumi wa buluu na kuunda wizara maalumu itakayosimamia eneo hilo, amepata mafanikio katika karibu kila sekta.

Kwa takribani wiki nzima, imezinduliwa miradi mbalimbali katika sekta za elimu, uwezeshaji na uwekezaji, huku Rais Mwinyi akihusika kufungua miradi hiyo.

Licha ya awali uchumi wa buluu kutoeleweka kwa wengi, sera yake hiyo sasa inatajwa kuanza kuleta mabadiliko na kuwa miongoni mwa sekta zinazotajwa kufanya vizuri.

Mwenyewe Dkt Mwinyi akizungumza Novemba Mosi, 2024 wakati wa kufungua Shule ya Sekondari ya Konde, Kaskazini Pemba, Rais Mwinyi alisema atawaonyesha watu kwa vitendo na dhamira yake ipo palepale kuibadilisha Zanzibar.

"Wengi walidhani hatutaweza, lakini haya tunayofanya ni salamu tosha, tumeahidi tumetekeleza na tutaendelea kutekeleza mengi bado yanakuja," alisema.

Mawaziri kadhaa, wakinukuliwa na gazeti la Mwanachi katika makala moja iliyochapwa Novemba 2, wameelezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika miaka minne ya Rais Mwinyi.

Katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Waziri Shaaban Ali Othman alisema uzalishaji wa samaki uliongezeka kwa asilimia 110.2 kutoka tani 38,107 zenye thamani ya Sh205.35 bilioni mwaka 2020 hadi kufikia tani 80,085 zenye thamani ya Sh569.07 bilioni mwaka 2023.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), walipokutana na Mwenyekiti wa The Islamic Foundation (TIF), Aref Nahdi, Ikulu Zanzibar kujadili jinsi ya utekelezaji wa miradi mbali mbali visiwani humo ikiwemo uchimbaji visima virefu 14 vya maji.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi (katikati) akikata utepe kama ishara ya ufunguzi wa Masjid Muhammed Bin Ahmed Al Jofair uliopo Chuini Wilaya ya Magharibi A Unguja, uliojengwa kupitia Wafadhili na Waislamu mbali mbali .

Alisema ongezeko hilo la shughuli za uvuvi limetoa ajira kwa wastani wa watu 63,000 ambapo asilimia 17 ni wanawake. Shaaban alisema mafanikio pia yamepatikana katika uzalishaji wa mwani uliongezeka kwa asilimia 89.6.

10,000

Mafanikio mengine makubwa ndani ya kipindi hicho ni kukamilika ujenzi wa soko la barafu la kisasa la samaki katika eneo la Malindi, ambalo kwa sasa linahudumia wastani wa watu 10,000 kwa siku na boti 350 za uvuvi.

Alisema mafanikio katika uvuvi ni matokeo ya mradi wa kugawa boti za uvuvi na mwani 1,027, Unguja ikipata 385 na Pemba 642, ambazo zimenufaisha wananchi 32,000, kati ya hao asilimia 7 ni vijana huku asilimia 90 ya boti za ukulima wa mwani wanufaika ni wanawake," alisema Shaaban.

"Jumla ya wakulima 1,001 Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya ukulima wa mwani katika kina kirefu kwa kutumia njia ya kamatia chini na vifaa vya kulimia mwani kwa kushirikiana na Kampuni ya Mwani Zanzibar (Zasco)" alisema.

Eneo jingine ambalo mafanikio makubwa yamepatikana ni katika ujenzi na ugawaji wa wa mashamba 100 ya kufugia majongoo bahari, mashamba 60 kwa ufugaji wa kaa na mashamba 20 ya ufugaji wa samaki.

Minne madarakani, rekodi za Rais Mwinyi zambeba

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwenye uzinduzi wa fursa za uchimbaji mafuta na gesi Zanzibar

Kutokana na juhudi hizo za uwezeshaji, mapato yatokanayo na tozo katika sekta ya uvuvi, kwa mujibu wa Waziri Shabani, yameongezeka kwa asilimia 262.5 kutoka Sh1.65 bilioni mwaka 2021 hadi kufikia Sh6 bilioni mwaka 2023.

Eneo linalotoa matumaini zaidi ni katika uchimbaji mafuta na gesi asilia, ambapo Shaaban alisema tayari wametangaza na kusimamia duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vinane vya mafuta na gesi asilia baharini kwa ajili ya uwekezaji katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Mafanikio mengine makubwa ndani ya kipindi hicho ni kukamilika ujenzi wa soko la barafu la kisasa la samaki katika eneo la Malindi, ambalo kwa sasa linahudumia wastani wa watu 10,000 kwa siku na boti 350 za uvuvi.

Upande wa viwada, Shaaban alisema Serikali imejenga kiwanda cha kusarifu mwani katika eneo la Chamanagwe, Pemba chenye uwezo wa kuchakata tani 30,000 za mwani mkavu kwa mwaka. Pia imejenga kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki katika eneo la Kama chenye uwezo wa kuzalisha tani tano za chakula cha samaki kwa siku.

Katika sekta ya elimu, mabadiliko yameanza kuonekana kwa upande wa ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa, lambayo huko nyuma shule za Zanzibar zilipata umaarufu kwa kufelisha wanafunzi wengi.

Kwa mujibu wa takwimu, ufaulu wa wanafunzi wa vipawa na michepuo katika mtihani wa darasa la saba umeongezeka kutoka asilimia 5.5 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 27.5 mwaka 2023, kidato cha pili umeongezeka kutoka asilimia 76.8 hadi 94.6%, na kidato cha nne umeongezeka kutoka 55.4% hadi 85.6% mwaka 2023 na kidato cha sita umeongezeka kutoka 96.2% hadi 99.6% mwaka 2024.

Mikakati kadhaa imetajwa kuleta mabadiliko hayo, ikiwa ni pamoja na kuongezea bajeti sekta ya elimu, ambapo kwa mwaka 2024/25 imepewa Sh830 bilioni kati ya Sh5.18 trilioni ikiwa ndiyo sekta inayoongoza kuliko zote.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa alisema bajeti ya maendeleo ya elimu imeongezeka kutoka Sh19 bilioni mwaka 2020 hadi kufikia Sh518 bilioni mwaka 2024.

"Uandikishaji wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 535,467 mwaka 2020 hadi kufikia wanafunzi 620,609 katika ngazi zote za elimu. Jumla ya watoto 35,941 walirejeshwa shuleni kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita," alisema.

Kwa upande wa miundombinu, serkali imejega shule za kisasa katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ili kuleta mageuzi katika sekta hiyo.

Hadi sasa, alisema shule za ghorofa 35 na madarasa 2,738 yamejengwa kwa kipindi cha miaka minne, huku serikali shule 91 zikifanyiwa ukarabati. Aidha, shule nyingine 26 za ghorofa, 53 za chini na madarasa mengine mapya 2,037 ujenzi wake tayari umeanza kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Akizungumzia suala la ajira, Lela alisema wizara imeajiri walimu 73 kwa upande wa mahitaji maalumu na kujenga vyuo vya amali vitano Unguja na Pemba ili vijana waweze kujiajiri.

Dk Mwinyi aliapishwa Novemba 2, 2020 kuingia madarakani baada ya kumshinda aliyekuwa mshindani wake wa karibu wakati huo, hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Bandari

Radio Imaan FM

Dar es Salaam **104.5fm**

Arusha **90.8fm** | Mwanza **106.5fm**

Mbeya **90.3fm** | Tabora **101.6fm**

Ruvuma **94.2fm** | Mtwara **90.9fm** | Kigoma **92.5fm**

96.3 Morogoro

Elimu Bila Mipaka

جُمادى الأول

HAPA NA PALE
NA SARAH ZUBERI

Rais Samia aondoa kero usafiri ziwa Victoria, meli mpya 2025

Maboresho makubwa yanayoendelea katika bandari za Kemondo, Bukoba, na Mwanza Kaskazini yanatarajiwa kuongeza ufanisi wa sekta ya usafirishaji katika eneo hilo.

Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Erasto Lugenge amesema kuwa ujenzi wa bandari ya Kemondo umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kukamilika hivi karibuni, huku mradi wa Bandari ya Bukoba ukiwa umekamilika kwa asilimia 75. Miradi hii ya maboresho yenye thamani ya zaidi ya Sh40 bilioni inatarajiwa kukamilika Novemba 2024.

Maboresho hayo yanahusisha kuimarisha kina cha maji, kuongeza urefu wa gati, na kujenga miundombinu ya kisasa kwa ajili ya abiria na mizigo. Vilevile, huduma za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na idara nyingine muhimu zitapatikana kwa urahisi kupitia vituo vya huduma vya sehemu moja. Maboresho haya pia yanatarajiwa kuboresha usalama wa bandari na kuongeza ufanisi wa huduma kwa wasafiri na wafanyabiashara.

Meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu, yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo, na magari makubwa na madogo, inatarajiwa kuanza kazi mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni

HABARI KWA UFUPI

Wagonjwa 60% Mwanza wana shinikizo la damu

Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 60 ya wagonjwa wanaofika hospitalini Mwanza wanakabiliwa na shinikizo la damu, hali inayotokana na ulaji usiofaa, ukosefu wa mazoezi, na mtindo wa maisha usio na afya. Shinikizo la damu ni moja ya vyanzo vikuu vya maradhi ya moyo, na hivyo wataalamu wa afya wameanza kutoa elimu na huduma za karibu kukabiliana na changamoto hii.

Kwa kutambua ongezeko la maradhi ya moyo, wataalamu kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wameanzisha kambi maalumu ya siku tano katika Hospitali ya Sekou-Toure, Mwanza, kutoa huduma za matibabu na ushauri kwa wagonjwa wa moyo. Kambi hii itapunguza mzigo wa gharama kwa wagonjwa ambao wangepaswa kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa huduma maalum.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana, ametoa wito kwa wakazi wa Mwanza kujitokeza kwa wingi kufaidika na kambi hii, akisisitiza umuhimu wa kufanyiwa vipimo na kubadilisha mtindo wa maisha ili kudhibiti shinikizo la damu.

Watahiniwa kidato cha nne Dar wakusanywa kupewa nasaha

Zaidi ya wanafunzi 1,500 kutoka wilaya zote za mkoa wa Dar es salaam wamejitokeza kwa wingi katika hafla ya kupeana nasaha a na dua ya pamoja kwa ajili ya watahiniwa wa kidato cha nne iliyoandaliwa na mzee Mikidadi Halfani mlezi wa wanafunzi wa kiislam mashuleni . Akizungumza na wanahabari baada ya dua hiyo, sheikh Salimu Baqir, amewaasa vijana hao kujikita katika uchamungu na hivyo kuwa karibu na Mola wao ili awawepesishie njia ya kufikia malengo yao kielimu. Pia aliwaasa kuacha kuangalia mambo yasiyofaa kupitia mitandao ya kijamii na kuacha kuiga mambo ambayo yapo kinyume na maadili ya Kiislamu. Aidha, Baqir, amesema dua ni muhimu kwa kila mtu, katika kutaka msaada wa Mwenyezi Mungu.

Kwa upande wao, wadau wa maendeleo kutoka taasisi ya elimu ya TESA, Mwalimu Nurdin Athumani, amesema taasisi yao imekuwa ikitoa fursa ya udhamini wa masomo kwa wanafunzi wa Kiislamu waliopata ufaulu mzuri ili wasome katika shule zenye misingi na maadili ya kiislamu.

Jenerali David Musuguri aagwa, aenziwa

Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango mwishoni mwa wiki hii aliwaongoza wakazi wa Dar es Salaam kuaga mwili wa aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Mstaafu David Musuguri, aliyefariki Oktoba 29, 2024, akiwa na umri wa miaka 104. Mwili wake uliagwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo, ambapo Dkt. Mpango aliwataka Watanzania, wakiwemo askari na raia, kujitoa kwa uzalendo kwa ajili ya kulinda uhuru, heshima, na maslahi ya taifa.

Dkt. Mpango aliwasisitiza vijana wa Tanzania kuwa na mapenzi ya dhati kwa nchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), na kuwa tayari kuilinda nchi kwa gharama yoyote, akisema kuwa Jenerali Musuguri ameacha mfano wa uzalendo na kujitoa kwa taifa. Alikumbusha mchango wa Jenerali Musuguri wakati wa vita dhidi ya utawala wa Idi Amin wa Uganda mwaka 1978, ambako aliongoza vikosi vya Tanzania kulinda mipaka ya nchi. Mwili wa Jenerali Musuguri umesafirishwa kwenda kijijini kwake Butiama, mkoani Mara, kwa ajili ya mazishi yatakayofanyika Jumatatu. Jenerali Musuguri alihudumu katika jeshi kuanzia mwaka 1942 hadi 1988, akiweka historia ya ushujaa na uongozi, na aliwahi kushiriki katika Vita vya Pili vya Dunia.

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

جُمادى الأول

/islamicftz

HABARI
NA SULEIMAN MAGALI

Shule za Imaan ufaulu juu darasa la saba

Shule ya awali na msingi ya Imaan iliyo chini ya taasisi ya The Islamic Foundation ya Mjini Morogoro, imeendeleza makali yake baada ya kufanikiwa kufaulisha wanafunzi kwa wastani wa daraja A

Wahitimu wa shule hiyo ambayo imekuwa mstari wa mbele katika utoaji wa elimu yenye maadili mazuri, taaluma na nidhamu wamepata A 62 kati ya watahiniwa 66 na kuifanya shule kupata wastani wa 261.3333

Shule hiyo imefanya kufanya vizuri ukilinganisha na mwaka jana ambapo takwimu zinaonesa katika watoto 47 waliosajiliwa, ni watoto 17 pekee walioweza kupata daraja A na wengine walipata daraja B.

Kwa upande wake, Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Ashraf Abdallah Abdul amesifu jitihada za uongozi wa taasisi ya The Islamic Foundation chini ya Mwenyekiti wake Aref Nahdi kwa jitihada kubwa wanazofanya kuhakikisha elimu bora inatolewa Ashrafu alisema matokeo mazuri ya shule hiyo ni matokeo ya ushirikiano wa wazazi, walimu, wanafunzi na utawala, na kwamba jambo hilo limekuwa likisimamiwa vizuri na kupelekea shule hiyo kuwa na matokeo chanya mwaka hadi mwaka

Ashrafu aliwasisitiza wazazi kuendelea kuziamini shule zinazofundisha wa misingi ya dini kwani watoto wakifahamu elimu ya dini itakuwa rahisi katika kumtambua mola wao na dira ya maisha yao

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Imaan, Swaleh Bahanzika, amesema siri ya mafanikio ya shule yake ni ushirikiano uliopo kati ya uongozi wa shule, walimu na wazazi

Pia amesema ulezi unaofanywa na taasisi ya The Islamic Foundation chini ya Mwenyekiti wake Aref Nahdi umekuwa chachu ya mafanikio kwa shule kwani wamekuwa mstari wa mbele kuwezesha shughuli mbalimbali za kiutendaji

“Tunaupongeza uongozi wa TIF kwa uwekezaji wake mkubwa iliyofanya katika shule hii, baada ya Mwenyezi Mungu, TIF wanafuata katika kufanikisha harakati za shule hii,” alisem Bahanzika.

Mafia Imaan yapata ufaulu wa A

Vilevile shule ya Mafia Imaan ambayo inamilikiwa na TIF imefanya vizuri katika mitihani yake, ambapo imeweza kupata wastani wa alama 244.9189.

Shule hiyo ambayo iko mkoa wa Pwani ilisajili watoto 37, ambapo kati yao 22 wamepata daraja A huku 15 wakipata daraja B.

Ufaulu naonyesha masomo ya Hisabati, Kiswahili, na Kingereza watoto wamefanya vizuri na kupelekea shule kupata wastani wa A, huku masomo ya Maarifa ya jamii na Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia pamoja na Uraia na Maadii wakipata daraja B.

Katika matokeo ya jumla, kwa mujibu Katibu Mtendaji NECTA Dkt. Said Mohamed, jumla ya watahiniwa 974,229 sawa na 80.87% ya watahiniwa wenye matokeo wamefaulu na kumaliza elimu ya msingi 2024.

Pia, alisema ufaulu wa jumla umeongezeka kwa 0.29% ukilinganisha na mwaka jana. Kati ya watahiniwa hao wavulana ni 449,057 sawa na 81.85% na wasichana ni 525,172 sawa na 80.05%.

Vilevile uchambuzi unaonyesha kuwa ufaulu wa wasichana umeshuka kwa 0.53% na ufaulu wa wavulana umeongezeka kwa 1.26%.

Kenya yapata naibu Rais mpya



Aliyekuwa waziri wa usalama wa ndani nchini kenya Profesa Kithure Kindiki ameapishwa rasmi kuwa naibu rais mpya wa Kenya akichukua mahala pa Rigathi Gachagua aliyeondolewa madarakani.

Kindiki anachukuwa wadhfa huo baada ya siku kadhaa za makabiliano ya mahakamani kati ya mawakili wa aliyekuwa naibu wa rais Rigathi Gachagua na wale wa serikali.

Gachagua alikwenda mahakamani kuzuia kuapishwa kwa Kindiki baada ya kudai kwamba aliondolewa madarakani kinyume na sheria, ombi lililokataliwa.

Katika hafla ya kuapishwa iliyofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Kenyatta (KICC) jijini Nairobi, Kithure aliahidi kuwahudumia Wakenya kwa moyo wake wote na alimshukuru rais William Ruto kwa kumteua kuwa naibu wake.

جُمادى الأول

KIMATAIFA

NA NYAMGUMA MAHAMUDU

Mkutano nchi za Kiislamu kuleta nusra Palestine au siasa

Saudi Arabia itakuwa mwenyeji wa mkutano wa pamoja wa nchi za Kiarabu na Kiislamu uakaofanyika Novemba 11 kujadili mashambulizi ya Israel Palestina na Lebanon pamoja na maendeleo mengine ya kanda hiyo, shirika la habari la Anadolu limeripoti.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya taifa hilo la Kifalme imesema mkutano huo utaendelea na mjadala ulioanzwa katika mkutano uliopita uliofanyika Riyadh tarehe Novemba 11, 2023, kujadili vita vya Israel dhidi ya Gaza.

Wachambuzi wa kisiasa wamekuwa wakijiuliza kama kutakuwa na jpya katika mkutano huo au ni muendelezo wa siasa za matamko, kuibembeleza Israel iache jinai ya mauaji ya kimbari ilhali huo ndiyo msingi mkuu wa uundwaji wake? Au itakuwa ni maombi mengine kwa Marekani iingilie kati, ilhali ishaweka wazi msimamo wake kwa vitendo wwa kuunga mkono Israel kwa hali na mali, bila kujali inatenda dhambi gani?

Katika taarifa ya Wizara hiyo ikitangaza mkutano huo imekemea 'uhalifu na ukiukwaji' wa haki unaoendelea kufanywa na Israel dhidi ya Wapalestina, pamoja na mashambulizi katika Lebanon, ikionyesha hatari kubwa kwa usalama na utulivu wa kanda hiyo.

Hata hivyo, Israel tayari imechagua kuwa kiziwi, ikipuuza makemeo dhidi yake siyo tu kutoka kwa nchi moja moja bali hata kwa taasisi kuu za kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa (UN) ambao azimio lake namba 181 la mwaka 1947 lililopitishwa na Baraza Kuu ndiyo lilikuwa ndiyo msingi wa uundwwaji wa taifa la Israel.

Katika mazingira haya, wachambuzi wa mambo wanasema mafanikio ya mkutano huu ni katika kuchukua uamuzi mgumu wa aidha uingiliaji kati wa kivita au vikwazo na kuacha kabisa ushrikiano wowote na Israel.

Vitisho vya kikanda vimeongezeka kutokana na mashambulizi makali ya Israel dhidi ya Ukanda wa Gaza, yaliyopelekea vifo vya zaidi ya watu 43,160, wengi wakiwa wanawake na watoto, kufuatia shambulio la Hamas mwaka uliopita. Kadiri mgogoro unavyoenea Lebanon, Israel imeendelea kufanya mashambulizi makali katika nchi hiyo, na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 2,700 na wengine zaidi ya 12,500 wakijeruhiwa tangu mwaka jana, kulingana na mamlaka za afya za Lebanon.

Licha ya maonyo ya kimataifa kwamba eneo la Mashariki ya Kati linakaribia vita vya kikanda kutokana na mashambulizi yasiyo na kikomo ya Israel dhidi ya Gaza na Lebanon, Tel Aviv ilipanua mgogoro huo tarehe 1 Oktoba kwa kuanzisha mashambulizi ya ardhini kusini mwa Lebanon.

Israel yapiga marufuku shirika la misaada la UN Palestina

Jumatatu (Oktoba 28) bunge la Israel (Knesset) lilipiga kura kuunga mkono miswada ya sheria inayopiga marufuku Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA).

Miswada hiyo iliyoidhinishwa na wabunge wa Israel 92 na kukataliwa na wabunge 10 inakataza mamlaka ya nchi hiyo kuwa na mawasiliano yoyote na UNRWA, na kulizuia shirika hilo kufanya kazi ndani ya Israel yenyewe.

Kupitishwa kwa msaada huko Gaza na Ukingo wa Magharibi kunahitaji uratibu wa karibu kati ya UNRWA na mamlaka ya Israeli. Hivyo, iwapo sheria hiyo itatekelezwa Israeli haitawapa tena wafanyakazi wa UNRWA vibali vya kazi au vya kuingia, na uratibu na jeshi la Israeli, muhimu kwa upitishaji salama wa usaidizi, hautawezekana tena.

Wanasiasa wa Israel kwa muda mrefu wamekuwa wakiikosoa UNRWA, huku wengine wakidai kuwa wafanyakazi wa shirika hilo wanashirikiana na Hamas. Madai hayo, ambayo yamekanushwa na shirika hilo, yameongezeka tangu mashambulizi ya Oktoba 7 yaliyoongozwa na Hamas dhidi ya Israel, ambapo zaidi ya watu 1130 waliuawa.

Katika mkutano na Baraza la Usalama mwezi huo, Kamishna Mkuu wa UNRWA, Philippe Lazzarini, alieleza kuwa shirika hilo ni "mhimili" wa operesheni nzima ya misaada huko Gaza, katika kukabiliana na "kampeni ya hila" ya mamlaka ya Israel kuisukuma nje ya ardhi za Palestina zinazokaliwa kwa mabavu.

UNRWA ilianzishwa muda mfupi baada ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa wenyewe kwa Azimio 302 la Baraza Kuu (IV), kufuatia vita vya Waarabu na Israeli vya mwaka 1948. Kwa miongo kadhaa, UNRWA imetoa huduma muhimu za kibinadamu kwa wakimbizi wa Kipalestina katika maeneo yanayodhibitiwa na Israel, hasa katika maeneo ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu (Ukingo wa Magharibi na Ukanda wa Gaza). Hizi ni pamoja na vituo vya afya, shule na vituo vya mafunzo ya ufundi stadi.

Wakati habari zikitokea Jumatatu, maafisa kadhaa wakuu wa Umoja wa Mataifa, hadi Katibu Mkuu, Antonio Guterres, walilaani uamuzi huo.

Bwana Guterres alimweleza Rais wa Baraza Kuu kwamba amemwandikia barua Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akiitaka serikali yake kuendelea kuruhusu UNRWA kufanya kazi, na kuheshimu wajibu wa Israel chini ya sheria za kimataifa.

Mashirika ya kibinadamu yazidi kuwapambania Warohingya



Mashirika ya haki za binadamu yameendelea kuweka shinikizo la kupatikana kwa haki za jamii ya Waislamu wa Rohingya ambao wamekumbana na mzozo mkubwa wa kibinadamu toka mwaka 2017.

Zaidi ya wakazi 700,000 wa Rohingya, wengi wao wakiwa ni Waislamu, walilazimika kukimbilia Bangladesh mwaka 2017 kutokana na mashambulizi makali ya kijeshi dhidi yao yaliyofanywa na majeshi ya Myanmar.

Katika mkasa huo, vikosi vya usalama vya Myanmar waliwatesa vikali Warohinya kwa kuwachomea nyumba zao, kuwabaka wanawake, na kuwaua.

Mashambulizi haya ya mwaka 2017 yameibua mashtaka ya uhalifu wa kivita na mauaji ya kimbari, na mashirika ya haki za binadamu yamekuwa yakidai haki kwa jamii hii ya Rohingya. Kwa mujibu wa taarifa kutoka mashirika ya wakimbizi, jamii ya Rohingya imekuwa ikiteseka na kukataliwa katika maeneo yao ya asili, huku maelfu wakihofiwa kupoteza maisha katika harakati za kuhama.

Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) huko The Hague imekuwa ikichunguza mashambulizi haya tangu mwaka 2019. Kesi hii inatarajiwa kuangalia vitendo vya ukandamizaji dhidi ya Waislamu wa Rohingya, ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa madai ya mauaji ya halaiki na mateso ya makusudi yaliyofanywa dhidi yao.

Kufuatia shinikizo la kimataifa na maandamano ya kuunga mkono Warohingya, mataifa mengi yamekuwa yakiitaka Myanmar kuacha ukandamizaji na kuipa haki jamii hiyo ya kurejea katika ardhi yao wakiwa salama.

Hata hivyo, mpaka sasa hakuna hatua madhubuti iliyochukuliwa na serikali ya Myanmar kurekebisha hali hiyo huku malaki ya Warohingya huko Bangladesh yakibaki ukimbizi.

Mashirika ya kibinadamu, hata hivyo, yameendelea kuwapa msaada wa kibinadamu huku yakipaza sauti kuiomba jamii ya kimataifa kuishinikiza Myanmar kuwajibika na kuruhusu Warohingya kurejea nyumbani kwao kwa amani na usalama.

Trump au Harris? Waislamu Marekani katika chaguo gumu

Jumanne ya Tarehe 5 Novemba Marekani inaingia katika uchaguzi wake mkuu ambapo rais wa zamani wa nchi hiyo Donald Trump atachuana na Makamu wa Rais wa sasa Kamala Harris.

Katika kipindi hiki, vifo na uharibifu Gaza na Lebanon bado unaendelea kushuhudiwa, Wamarekani wenye asili ya Kiarabu na Waislamu wanakumbana na ugumu mkubwa wa kuamua nani wampe kura zao.

Wakati mgogoro wa Mashariki ya Kati unapoendelea, Waislamu wengi wa Marekani, waliomuunga mkono Rais Joe Biden miaka minne iliyopita, wanasita kuendela kuunga mkono chama chake cha Democrats, kufuatia uamuzi wa serikali yake kuunga mkono Israel kwa kuipatoa silaha zinazotumika kuua Wapalestina.

Kwa kitendo hicho, Waislamu wanahisi wamepuuzwa na kusalitiwa, hata hivyo wametofautiana juu ya nini cha kufanya.

Baadhi ya Waislamu wanaona ipo haja ya kukikataa chama cha Democrats huku wengine wakitafakari juu ya kumuunga mkono mgombea wa chama cha tatu. Hata hivyo, wakifikiria kwa makini zaidi Waislamu pia wanaingiwa hofu juu ya uwezekano wa hasira zao kumrahisishia njia ya kurejea Ikulu ya Marekani. Trump hajawahi kuficha chuki yake kwa Uislamu na Waislamu.

Kwa wapiga kura wa majimbo muhimu kama Georgia, ambako Biden alishinda mwaka 2020 kwa kura chache, uamuzi wa kura hizi una uzito mkubwa. Shafina Khabani, Mkurugenzi Mtendaji wa Georgia Muslim Voter Project, anasema majibu yanatofautiana sana, na hayana uelekeo mmoja wa kisiasa kama zamani. Khabani anaeleza kuwa jamii yake imejawa na huzuni, uchungu, na hasira huku ikipitia wakati mgumu wa maamuzi.

Katika kampeni ya hivi karibuni inayojulikana kama “Hakuna Amani Hakuna Kura”, Waislamu nchini humo walitoa wito wa kujizuia kumpigia kura mgombea yoyote mpaka awathibitishie kuwa atasitisha msaada wa kijeshi kwa Israel. Waislamu wengi wanaona umuhimu wa kuikumbuka Palestina wakati wa kupiga kura na kuchagua kwa dhamiri zao. Latifa Awad, ambaye ana ndugu Gaza, alisema anataka kupiga kura kwa Jill Stein ili kutoa ujumbe kwamba sauti zao zina umuhimu.

Majimbo muhimu kama Michigan yanashuhudia mgombea Trump akipata uungwaji mkono kutoka kwa Waislamu, ikiwemo kutoka kwa mameya wawili. Waislamu wa Marekani wanatarajiwa kufanya tofauti katika majimbo haya muhimu, huku wakihimizwa kuzingatia wagombea watakaoleta mabadiliko.

UN: Mauaji ya waandishi duniani yaongezeka kwa 38%

Ripoti ya Shirika moja la Umoja wa Mataifa iliyotolewa Jumamosi inaonyesha kwamba mauaji ya waandishi wa habari kote duniani yaliongezeka katika mwaka wa 2022 na 2023 ikilinganishwa na miaka miwili kabla ya awali.

Ripoti hiyo ya Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Utamaduni UNESCO inaonyesha kuwa waandishi 162 waliuwawa wakiwa kazini hiyo ikiwa ongezeka la asilimia 38.

UNESCO kupitia kwa mkurugenzi wake mkuu Audrey Azoulay inasema ongezeko hilo la mauaji linatia hofu kwani hakuna hatua iliyochukuliwa katika karibu visa vyote hivyo vya mauaji.

Azoulay ameyataka mataifa duniani kuongeza juhudi kuhakikisha kwamba wanaotenda vitendo hivyo vya kihalifu vya kuwauwa waandishi wanachukuliwa hatua. Katika kipindi cha miaka miwili hiyo, kanda ya Amerika Kusini na visiwa vya Caribbean ndizo zilizoshuhudia mauaji mengi ya waandishi, 61 wakipoteza maisha.

Kulingana na UNESCO maeneo ambayo hayana hatari kubwa kwa waandishi ni Amerika Kaskazini na Ulaya Magharibi ambapo waandishi 6 pekeyake ndio waliouwawa katika kipindi hicho cha miaka miwili.

HABARI KWA UFUPI

Israel yapiga marufuku shirika la misaada la UN Palestina

Jumatatu (Oktoba 28) bunge la Israel (Knesset) lilipiga kura kuunga mkono miswada ya sheria inayopiga marufuku Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA).

Miswada hiyo iliyoidhinishwa na wabunge wa Israel 92 na kukataliwa na wabunge 10 inakataza mamlaka ya nchi hiyo kuwa na mawasiliano yoyote na UNRWA, na kulizuia shirika hilo kufanya kazi ndani ya Israel yenyewe.

Kupitishwa kwa msaada huko Gaza na Ukingo wa Magharibi kunahitaji uratibu wa karibu kati ya UNRWA na mamlaka ya Israeli. Hivyo, iwapo sheria hiyo itatekelezwa Israeli haitawapa tena wafanyakazi wa UNRWA vibali vya kazi au vya kuingia, na uratibu na jeshi la Israeli, muhimu kwa upitishaji salama wa usaidizi, hautawezekana tena.

Wanasiasa wa Israel kwa muda mrefu wamekuwa wakiikosoa UNRWA, huku wengine wakidai kuwa wafanyakazi wa shirika hilo wanashirikiana na Hamas. Madai hayo, ambayo yamekanushwa na shirika hilo, yameongezeka tangu mashambulizi ya Oktoba 7 yaliyoongozwa na Hamas dhidi ya Israel, ambapo zaidi ya watu 1130 waliuawa.

Katika mkutano na Baraza la Usalama mwezi huo, Kamishna Mkuu wa UNRWA, Philippe Lazzarini, alieleza kuwa shirika hilo ni "mhimili" wa operesheni nzima ya misaada huko Gaza, katika kukabiliana na "kampeni ya hila" ya mamlaka ya Israel kuisukuma nje ya ardhi za Palestina zinazokaliwa kwa mabavu.

Israel yatia fora kwa kuwa na kesi nyingi ICJ

Kesi zlizosajiliwa zimeongezeka maradufu katika Mahakama ya Kimataifa ya haki (ICJ), jambo linaloashiria kuongezeka kwa mgawanyiko wa kimataifa na umuhimu wa kuwepo chombo huru kisichoegemea upande wowote ili kushughulikia migogoro ya kisheria kati ya nchi. Msajili wa Mahakama hiyo, Philippe Gautier, akihojiwa na UN News, amesema Mahakama inakabiliwa na kesi 23, idadi ambayo haijawahi kushuhudiwa hapo awali.

Kati ya hizo, nane zinahusiana moja kwa moja na Mashariki ya Kati, zikiwemo kesi zinazohusisha mkataba wa kimataifa wa kuzuia mauaji ya kimbari na sheria za kibinadamu. Gaza imekuwa kitovu cha baadhi ya kesi hizi, huku Afrika Kusini ikiishtaki Israel na Nicaragua ikiishtaki Ujerumani kwa kutoa silaha zinazokiuka mikataba ya kimataifa.

Wakati idadi ya kesi ikiongezeka, Gautier anaamini kuna jambo la msingi zaidi linalojitokeza. "Kila wakati nchi inapoleta kesi ICJ, ni ushindi kwa ushirikiano wa kimataifa. Hii inaonesha matumaini katika mfumo wa kimataifa ambao bado unaleta matokeo."

Katika maoni ya ushauri yaliyotolewa Julai kuhusu sera za Israel katika Maeneo ya Palestina Yanayokaliwa, ICJ ilisema kuwa uwepo wa muda mrefu wa Israel ni kinyume cha sheria. Gautier ameeleza kuwa maoni ya ushauri yanatolewa ili kutoa mwongozo wa kisheria kwa waombaji, lakini si lazima kuyatekeleza.

Mafuriko yaua zaidi ya 200 Hispania

Mafuriko makubwa zaidi yaliyotokea Uhispania yameua watu 205 huku Serikali ikipeleka askari 500 zaidi kusaidia katika harakati za kuwatafuta manusura.

Mafuruko hayo yameharibu magari, yamevunja madaraja na kuifunika miji na tope tangu Jumanne, yametajwa kuwa ndio janga kubwa kabisa la aina hiyo kutokea katika nchi hiyo ya Ulaya katika miongo mingi. Shirika linaloratibu huduma za dharura katika mkoa wa mashariki wa Valencia ulioathiriwa pakubwa limesema watu 205 wamethibitishwa kufa huko.

Idara ya hali ya hewa AEMET imeiweka sehemu ya kusini mwa Andalusia katika kiwango cha juu zaidi cha tahadhari ya mvua kubwa zaidi leo. Aidha imeyatahadharisha maeneo ya Valencia na Catalonia.

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

جُمادى الأول

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

Ufaulu la 7 uwe chachu ya kufanya vizuri sekondari

Jumanne wiki hii, Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) lilitangaza matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka huu, ambayo yanaonesha ufaulu umepanda kwa asilimia 0.29.

Taarifa ya Katibu Mtendaji wa Necta, Dkt. Said Mohamed inaonesha kwamba kati ya watahiniwa 1,204,899 waliofanya mtihani, watahiniwa 974,229 sawa na asilimia 80.87 wamefaulu, wakiwamo wavulana 449,057 sawa na asilimia 81.85 na wasichana 525,172 sawa na asilimia 80.05.

Sisi gazeti la Imaan tunawapongeza watahiniwa wote waliofanya vizuri katika mitihani yao na tunawatakia maandalizi mema ya kujiunga na kidato cha kwanza hapo mwakani.

Inafurahisha kuona kuwa kati ya watahiniwa 974,229 waliofanya mtihani huo, watahiniwa 431,689 wamepata daraja A na B. Hii ni hatua nzuri na kubwa kwa sababu itawapa ari na hamasa ya kusoma kwa bidii pindi watakapoingia sekondari.

Jambo la muhimu kwa sasa ni wanafunzi kuendeleza heshima na nidhamu waliyoionesha pindi walipokuwa shule ya msingi. Wakati wanafunzi wakisubiri kujiunga na kidato cha kwanza mwezi Januari mwakani, ni vizuri wazazi wakaanza

mipango ya kuwanunulia vifaa vya shule vikiwemo sare, mabegi, madaftari, peni, vitabu na vifaa vya kujifunzia.

Wataalamu wa saikolojia wanasema, mwanafunzi anapoona baba, mama au mlezi wake ameandaa kila kitu kinachohusu shule hujisikia furaha na hupata shauku ya kusoma. Hivyo tunaona kuwa upo umuhimu wa kununua vifaa vya shule mapema.

Kwa upande mwingine, wazazi wana wajibu wa kuwaelekeza watoto wao katika kutekeleza haki za Mola wao na vilevile kwa viumbe wake. Haki ya Mwenyezi Mungu ni kuabudiwa peke yake, na huo unapaswa kuwa wajibu wao siku zote wawapo shuleni au nyumbani.

Hivyo wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao wajibu huo ili kujiondoa kwenye dhima mbele ya Allah Ta'ala. Allah anasema katika Qur'an: "Enyi mliyoamini! Ziokoeni nafsi zenu na ahali (familia) zenu kutokana na Moto, ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayowaamrisha, na wanatenda wanayoamrishwa." [Quran, 66:6].

Na katika hadith aliyoisimulia Abdullahi bin Umar (Allah amridhie), mjumbe wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani zimshukie) amesema: "Nyote ni wachunga na kila mmoja wenu ataulizwa kuhusu alichokichunga. Kiongozi ni mchunga na ataulizwa kwa alichokichunga. Mwanaume ni mchunga wa familia yake na ataulizwa kwa alichokichunga. Mwanamke ni mchunga wa nyumba ya mume wake na watoto wake, naye ataulizwa kwa alichokichunga..." [Bukhari na Muslim].

جُمادى الأول

NASAHA ZA WIKI

NA YUSUFU AMINI

Utandawazi unavyozalisha kizazi kisichomhofu Mungu

"Mwacha mila ni mtumwa!" Huo ni usemi maarufu unaoelezea ubaya wa mtu kupuuza au kuacha kufuata mila, utamaduni au asili yake. Ndugu yangu Muislamu, usemi huu unaweza kuona ni wa kawaida, lakini una maana kubwa sana katika maisha yako hapa duniani.

Hebu itazame aya hii: "Na ni nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu? Na kwa yakini sisi tulimteua yeye (Ibrahim) katika dunia; na kwa hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema." [Qur'an, 2:130].

Pia itazame aya hii: "Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini yeye alikuwa mwongofu Muislamu, na hakuwa katika washirikina." [Qur'an, 3:67]. Katika aya hizi mbili kuna dalili inayothibitisha kwamba mila ya Ibrahim aliyoikusudia Allah ni Uislamu, yaani kumnyenyekea Allah peke yake kwa kumtii na kumuabudu.

Kumbe basi, kila aitwae Muislamu anatakiwa kuutekeleza Uislamu kikamilifu kwa kuwa ndiyo mfumo sahihi wa sheria, mila na utamaduni umfaao mwanadamu.

Hata hivyo, changamoto kubwa iliyopo ni jamii yetu kuathiriwa na utandawazi. Ni kweli kabisa, utandawazi umechangia pakubwa katika kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya watu, lakini kwa upande wa pili umeleta maafa makubwa duniani hasa upande wa maadili na tabia.

Mabadiliko ya kimaisha yaliyoletwa na utandawazi, kwa kiasi kikubwa yameharibu maana halisi ya maisha ya Kiislamu kwa baadhi ya Waislamu hususani vijana. Matokeo yake vijana wengi wamejikuta wanaiga na kukumbatia mambo maovu wanayoyaona kwenye televisheni na mitandao ya kijamii kwa kisingizio cha kwenda na wakati. Tena wanafanya hivyo pasina haya wala kujali kama wanamkosea Mungu.

Janga la zinaa

Miongoni mwa athari hasi zilizoletwa na utandawazi ni watu kuikurubia zinaa. Vijana wengi hivi sasa wanaonekana kuburudika na vishawishi vya zinaa kutokana na yale wanayoyashuhudia kwenye televisheni na mitandao ya kijamii.

Katika hali ya kushangaza, wakati viongozi wa dini wakipambana kukemea zinaa, taasisi na wanaharakati mbalimbali wamekuwa wakichochea zinaa kwa kufanya matamasha ya kuhamasisha 'ngono salama' na kuwagawia vijana mipira ya kiume na ya kike (kondomu) bure sambamba na kuwapa elimu ya kuitumia.

Jambo baya zaidi ni kuwa, jamii yetu imefikishwa mahala ambapo inaona uzinifu ni jambo la kawaida. Baadhi ya mitandao na vyombo vya habari vimekuwa vikiwanadi wazinifu na kutangaza maovu waliyofanya na wazinifu wenzao wa sasa na wa zamani (Ma–ex) kwa kiwango kikubwa.

Kupiga picha na kuziweka mitandaoni

Kila nikiperuzi mitandao ya kijamii nakutana na picha za wasichana na wanawake waliovaa mavazi yanayobana au kuonesha maungo yao, waliojipamba kwa wanja, rangi za midomo, kuvaa urembo shingoni, mikononi, masikioni, tena wakiwa hawajafunika vichwa vyao.

Inasikitisha na kushangaza kuona wanawake wengi, wakiwemo Waislamu wanafanya uovu huu kwa fahari kubwa. Subhanallah! Niwaulize dada zangu na mama zangu: "Mnafanya hayo yote kwa ajili ya nani?" Sababu yoyote mtakayotoa haiwezi kuhalalisha jambo hili.

Ninachokiona sasa ni wanawake wengi kucharuka katika kunadi miili yao mitandaoni, na kwa hakika hili ni jambo la kijinga lililokemewa vikali na Allah Ta'ala. Allah anasema kuwaambia wanawake: "Na kaeni kwenye nyumba zenu wala msidhihirishe mapambo kama walivyodhihirisha wanawake wa kale wa zama za ujinga." [Qur'an, 33:33].

Maana ya aya ni kwamba, mwanamke yeyote ajipambaye kwa aina yoyote ya mapambo kisha akaonesha mapambo yake kwa wanaume wasio maharimu zake, sheria inamzingatia kama mzinifu.

Nyimbo na miziki

Siku hizi ni vigumu sana kukaa sehemu bila kusikia sauti ya muziki. Kuna watu ambao ibada zao ni miziki, na wengi hususani vijana wamegeuza muziki kuwa njia ya kujipatia fedha za haraka haraka.

Wengine wameufanya muziki kama burudani kwao bila kujali uharamu. Allah Ta'ala anasema: "Na miongoni mwa watu wapo wanaonunua maneno ya upuuzi ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu pasipo kujua, na wanaichukulia ni maskhara. Hao watapata adhabu ya kuwafedhehesha." [Qur'an, 31:6].

Swahaba Abdullahi bin Mas'ud (Allah amridhie) aliulizwa kuhusiana na aya hii akasema: "Ni nyimbo. Naapa kwa yule ambaye hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye." Akarudia mara tatu, [Tafsir ya Qur'an Ibn Kathir].

Na katika hadith iliyonukuliwa na Bukhari, Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake) amesema: "Watakuja watu katika umma wangu watakaohalalisha hariri, pombe na vyombo vya muziki."

Kamari

Ukifanya utafiti mdogo utaona michezo ya kamari imepewa nafasi kubwa katika mitandao na vyombo vya habari, na watu wamehamasika kukimbilia huko wakichukulia kama njia ya kupata fedha kwa njia ya mkato. Vijana wanashindwa kutumia nguvu zao katika kumuabudu Allah na kuimarisha maisha yao, badala yake wamezama katika kamari na maasi mengine.

Haya yote yanatokea kwa sababu wazazi na jamii wameacha kukilea kizazi katika mafundisho ya dini. Malezi yanapasa kuzingatia mafundisho ya dini lakini wazazi wamepuuza na kushughulishwa na kuitafuta dunia.

Wazazi wanahangaika kuwafundisha watoto wao elimu ya mazingira na kuwaweka mbali na elimu ya kiroho. Matokeo yake jamii inapitia mitihani na matatizo yasiyokuwa na suluhisho.

جُمادى الأول

MALEZI NA FAMILIA

JUNAYNAT ALLY DAMA

Mlee binti awe mwanamke mchamungu ayejiamini

Tunaomba sana dua kwa Mwenyezi Mungu awakuze watoto waje kuwa wachamungu, lakini hii haiondoi ukweli kuwa sisi wenyewe wazazi tuna jukumu la kufanya katika kuwaelekeza, kuwafundisha na kuwaadabisha watoto wawe hivyo tunavyoota: watiifu kwa amri za Allah na Mtume wake, wanyenyekevu na wenye huruma kwa watu, wachapakazi, wakweli na waaminifu na kadhalika.
Hii ni makala yenye nukta kadhaa za ushauri kwa wazazi wa mabinti juu ya mbinu za kimalezi za kumjenga mwanao awe mwanamke mchamungu na mwenye mchango chanya kwa jamii.

Mosi, mfundishe kuipenda Hijab yake.

Mtihani mkubwa kwa mabinti unaanza kwenye uelewa wa dhana na hijab, kama ishara ya staha na kielelezo cha imani kwa wanawake wa Kiislamu. Asipovaa vazi hili la stara la Hijab, mbele ya watu wasio maharimu wake au wanawake wenzake, basi mwanamke anakuwa anatembea uchi. Kwa hiyo, ni muhimu binti afunzwe kuvaa vazi la hijab tangu mapema. Binti afundishwe kuwa kinyume cha fikra za wengi, hijab ni taji kwa mwanamke, na siyo kikwazo.

Mfundishe kujiheshimu

Binti afundishwe kujiheshimu katika kila nyanja: kwa mavazi, kauli na hata vitendo. Mtoto wa kike afunzwe kuwa uzuri wa kweli umejificha kwenye kujiheshimu.

Katika viengele vya kujiheshimu binti avae vazi la kisheria la hijab, ashushe macho yake, aulinde moyo wake, akae sehemu zinazoakisi heshima yake, awe na marafiki wema, asipayukepayuke katika kuongea mbele za watu na kucheka hovyo, asichaganyike na kugusana na wanaume wasio maharimu wake.

Imepokelewa hadith kutoka kwa Ibn 'Umar (Allam amridhie) kwamba Mtume wa Allah (rehema za Allah na amani zimshukie) alipita kwa mtu miongoni mwa Answaar akamnasihi akimnasihi nduguye kuhusu kuacha kuona haya. Mtume akasema: "Mwache, kwani haya ni katika imani". [Bukhari na Muslim]. Kama Muislamu yabidi awe na haya, mwanamke ni zaidi.

Msimamie achague marafiki wema

Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mtu yamkini kufuata dini ya rafiki yake, kwa hivyo muangalie unaemfanya rafiki." [Abu Dawud na Tirmidhi]. Katika hadith nyingine, amesema: "Mfano wa rafiki mwema na rafiki mbaya ni kama ule wa muuzaji wa miski na mhunzi. Basi kwa muuzaji wa miski, aidha atakunusisha, au utanunua kwake ama angalau utafurahia harufu nzuri kwake. Na kwa yule mhunzi, aidha atakuchomea nguo au utapata harufu mbaya kutoka kwake." [Bukhari na Muslim].

Kama marafiki wana ushawishi mkubwa kiasi hiki watu, bas bila shaka kwa watoto ni zaidi. Hivyo basi, ni jukumu la mzazi kumlinda bintiye dhidi ya marafiki wabaya.

Njia nzuri ya kumsaidia mtoto kutengeneza marafiki wazuri ni wewe mzazi kuwa na marafiki wazuri ambao utawaalika kama familia nyumbani. Kwa namna hiyo, utamkutanisha binti na mabinti wenzie kutoka katika familia zenye maadili sawa na familia yako.

Mpe fursa mtoto acheze

Mtoto wa kike naye anastahili kupata fursa ya kujihusisha na michezo, madhali haikiuki sheria na misingi ya Kiislamu. Binti anaweza kufundishwa kuogelea, kulenga shabaha, kupigana kama namna ya kujilinda, mpira wa kikapu, rede na michezo mingine mingi.

Michezo ni muhimu kwa sababu inachangamsha mwili, inamjengea binti hali ya kujiamini na tukumbuke kuwa mwili una haki yake. Mwili usioshughulishwa aghlab hugeuka kuwa jumba la maradhi.

Mfundishe kazi za nyumbani

Mwisho wa siku, inshaAllah, bint ataolewa na kuwa kiongozi wa nyumba yake, akilea familia. Haijalishi atakuwa nani katika masuala ya kazi – daktari, mwalimu, rais, mkurugenzi, mhandisi - majukumu ya kuilea familia yako palepale.

Kwa msingi huo, ni muhimu kumfundisha bint kazi za nyumbani ili akue akizizoea. Kutegemeana na umri, ajifunze usafi binafsi na wa nyumba, mapishi ya aina mbalimbali, kupanga bajeti ya familia, kuogesha watoto, kufua, kuosha vyombo na kadhalika.

Mfunze kupenda kujifunza

Mzoeshe mtoto kusoma vitabu. Anza kwa kumsomea, na akijua kusoma asome mwenyewe. Muombe akuhadithie simulizi kwenye vitabu. Ukiona vitabu vipya, mnunulie.

Kusoma ni moja tu ya njia za kujifunza mambo lakini zipo nyingine nyingi kama kuangalia televisheni na vyombo vya habari vya mtandaoni, vinavyomfaa na chini ya usimamizi.

Ni muhimu sana kumjengea mazingira ambapo kujifunza kwake kuwe kwa raha na burudani ili afurahie. Kwa namna hii, kujifunza ataimarika katika kupenda kujifunza hadi iwe tabia ya kudumu katika maisha yake.

Mfunze apende uanamke wake

Kuna tatizo siku hizi la wanawake kuchukia uanamke wao na kutaka kubeba tabia za kiume. Wapo wanaosema, kwa mfano, sitaki kuolewa wala kuomba ruhusa kwa mtu. Wengine wanavaa mavazi kama wanaume.

Huko ni kuchukia na kuikana heshima ambayo mwanamke kapewa na Mwenyezi Mungu kama msaidizi kwa mumewe ambao kwa pamoja wanakamilishana, kama mama, kama mlezi wa familia, na kama mwalimu wa kwanza.

Mtambulishe wanawake 4 bora

Ni vizuri watoto kukua wakiwa na watu wanawaangalia kama viigizo (role models). Kwa wanaume, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ni kiigizo chetu cha moja kwa moja kwa sababu yeye alikuwa mume, mlezi, kiongozi wa familia kama wanaume wetu hawa.

Kwa upande wa wanawake, wanawake wanne wametajwa kuwa bora zaidi kuliko wengine wote. Hawa ni wanawake wa Peponi moja kwa moja, kwa uwezo na mapenzi ya Allah. Mtambulishe binti yako kwa wanawake hawa, awajue habari zao na ajifunze kutoka kwao.

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

جُمادى الأول

/islamicftz

MAKALA

NA SAID RAJAB

SEHEMU YA TATU

Mtazamo wa Uislamu kuhusu upandikizaji mimba



Wiki iliyopita katika mfululizo wa makala hizi kuhusu mtazamo wa Uislamu juu ya upandikizaji mimba, tuliishia na kipengele cha urutubishaji wa yai kwa njia ya IVF ambapo tulieleza kuwa, ova iliyorutubishwa kwa mafanikio huhamishiwa kwenye tumbo la uzazi (uterus) la mke.
Tulisema, katika hatua hii tumbo la uzazi linakuwa tayari limeshatayarishwa na homoni kupokea na kuanza kupandikiza mimba hiyo iliyohamishwa. Sasa endelea na sehemu inayofuata...

Kiwango cha sasa cha mafanikio kinachopimwa kwa urutubishaji na kusababisha mtoto kuzaliwa akiwa hai ni kati ya asilimia 20 na 30.

IVF, pamoja na marekebisho yake mbalimbali, yaani 'Gamete Intra–fallopian Transfer' (GIFT), sindano ya manii ya intracytoplasmic (ICSI) na kadhalika, imetangazwa kuwa inaruhusiwa Kiislamu ikiwa tu masharti yafuatayo yatatimizwa.

Kwanza, upandikizaji mimba (IVF) lazima uhusishe wanandoa, pili mbegu za kiume (sperms) lazima zitoke kwa mume na mayai yatoke kwa mke, na tatu jambo hili lazima litokee wakati wanandoa wangali ndani ya ndoa yao halali.

Nne, mchakato huu lazima ufanywe na timu makini ya madaktari wenye uwezo ili kupunguza uwezekano wa kuchanganya mimba za wanandoa tofauti wakati zinapowekwa kwenye 'liquid nitrogen'.

Tano, mwanamke asiye katika ndoa husika asitumike kama chombo cha kuzaa mtoto kwa ajili ya wanandoa wengine. Mwisho, idadi inayofaa ya mayai yaliyorutubishwa ndiyo inapaswa kuhamishiwa kwenye tumbo la uzazi (uterus).

Ni kawaida kuhamisha mayai mawili hadi matatu tu yaliyorutubishwa, ingawa kwa kawaida kuna mayai mengi yaliyorutubishwa yanayozalishwa. Vituo vingi huhamisha yai moja au mawili tu yaliyorutubishwa.

Kugandisha mayai yaliyobaki yaliyorutubishwa inaruhusiwa na baadhi ya Wanazuoni wa Kiislamu ilimradi tu mayai hayo yatumike katika mizunguko inayofuata kwa wanandoa hao hao, tena wakiwa bado wamo ndani ya ndoa.

Hatima ya mayai ambayo hayajatumiwa bado haijaamuliwa, lakini inaruhusiwa kuyatumia kwa utafiti wa kimatibabu, kwa idhini ya wanandoa husika na kwa kuzingatia miongozo inayofaa. Hata hivyo, mwaka 1990 Chuo cha Kimataifa cha Fiqh ya Kiislamu cha Shirika la OIC–IFA kilikataa kabisa kugandishwa kwa viinitete (pre–embryos) kabla ya kutokea matukio ya kuchanganya mimba na viinitete.

Maoni ya Uislamu kuhusu teknolojia ya usaidizi wa uzazi

Mafundisho ya Qur'an na Sunna yamesisitiza jukumu muhimu la ndoa na muundo wa familia, ambapo tendo la uzazi haliwezi kutenganishwa na jambo hili. Kwa maana hiyo, Allah 'Azza wa Jallah' anasema katika sura ya An–Nahl (Qur'an, 16:72): "Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu watoto na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini upotovu na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?"

Uzazi bandia haukutajwa katika vyanzo vya msingi vya sheria ya Kiislamu, lakini iwapo uzazi wa kawaida unashindikana, Uislamu unahimiza matibabu kwa kuwa kuasili watoto siyo suluhisho linalokubalika.

Hivyo, majaribio ya kuponya ugumba si tu yanaruhusiwa bali pia yanahimizwa. Wajibu wa daktari ni kuwasaidia wanandoa wenye ugumba kufikia urutubishaji wa mafanikio, utungaji mimba na hatimaye kuzaa mtoto.

Teknolojia zote za usaidizi wa uzazi (ART) zinaruhusiwa katika Uislamu iwapo tu chanzo cha mbegu za kiume (spems), mayai (ovum) na mfuko wa uzazi (uterus) kinatoka kwa wanandoa halali, tena wakiwa ndani ya ndoa yao.

Kwa mujibu wa Uislamu, ugumba wa mwanaume au mwanamke unapaswa kukubaliwa ikiwa hauwezi kuponywa au kutibika. Usaidizi wa uzazi ulikubaliwa kwa kiasi kikubwa baada ya taasisi zenye heshima za kisayansi na kidini kutoa miongozo ambayo ilikubaliwa katika nchi tofauti za Kiislamu.

Wafundishe Watoto wako

kuwa Dini sio kikwazo,

bali ni **kinga.**

The Islamic Foundation

tvImaan Tanzania

Radio Imaan FM

IMAAN NEWSPAPER

www.islamicftz.org

جُمادى الأول

AFYA

JUNAYNAT ALLY DAMA

Tunza masikio lakini usitumie vijiti vya pamba

Kila mtu - hata wataalamu wa afya - watakuwa wamewahi kuzitumia wakati fulani klkini ni hatari na wala si jambo tunalolazimika kulifanya. Sikio lina utaratibu wa kujisafisha lenyewe kwa hiyo acha kulichokonoa kwa vijiti vya pamba, hata kama unasikia raha.

Tuwe wakweli. Ni nani asiyefurahia kuweka kijiti cha pamba kwenye sikio lake? Akakizungusha taratibu, kisha akakitoa nje na kukichunguza ncha nyeupe iliyozungushwa na pamba ikiwa imegeuka njano?

Tusichojua ni kwamba mkandamizo wa kijiti unaweza kusababisha madhara makubwa katika mfereji wa sikio au hata ngoma. Sikio linaweza kuziba kwa sababu ya kusukuma uchafu ndani au pamba kubaki ndani. Unaweza kupata maumivu, maambukizi, kutokwa damu kwa sababu ya kuchubuliwa na kadhalika.

Ukitoboa ngoma ya sikio, unaweza kusikia sauti zisizoeleweka lakini pia inaweza kupelekea uziwi. Bahati mbaya sana ni kuwa hadi watoto wanatumia vijti vya pamba na hivyo kuwaweka hatarini kupasua ngoma.

Nta ya sikio

Kuweka sikio safi ni muhimu ili kuepuka matatizo ya usikivu lakini ni ipi njia bora ya kusafisha masikio yako? Kabla ya kubu maswali haya, tujiulize uchafu unaotolewa sikioni ni nini?

Kuna kitu kinatwa nta ya sikio (earwax au cerumen) ambayo ni maji maji fulani mazito yaliyopo ndani ya sikio kwa kazi maalumu ya kulinda sikio dhidi ya hatari mbalimbali ikiwemo maambukizi, vumbi au uchafu mwingine.

Nta masikioni inakuwepo kwa kiwango maalumu lakini inaweze kuongezeka. Nta ikiwa katika kiwango cha kawaida, huhitaji kamwe kusafisha masikio kwa sababu sikio linajisafisha lenyewe. Hata hivyo, nta ikizidi utahitaji kuiondoa kwa tiba.

Unajuaje nta imezidi? Kuna dalili kadhaa ikiwemo kuhisi sikio zito, limejaa, limeziba, usikivu kupungia, kusikia sauti za ajabu ajabu, sikio kuuma, kuwasha na harufu. kizunguzungu, maumivu ya kichwa na kikohozi kikavu baada ya kuwashwa sikio pia ni katika dalili.

Tumesema kuchokonoa sikio kwa vijiti kunaweza kupelekea kuongezeka na kurundikana kwa nta sikioni, lakini hicho chanzo pekee. Maambukizi sikioni mara kwa mara, umbo la mfereji wa sikio kutoruhusu nta kutoka, uzee, kuogelea na matumizi ya spika za masikioni pia huchangia tatizo hilo.

Tiba ya bora ya nta kujaa au tatizo jingine la sikio ni kumuona daktari. Yeye atasikiliza dalili, atakupima na kuamua aidha kukupa dawa za kuweka sikioni kwa ajili ya kuyeyusha nta kisha itoke yenyewe. Kama dawa ikishindwa, ziko njia zingine kama kuilainisha nta na kuitoa kwa kutumia vifaa maalumu vya kitaalamu.

Usafi wa sikio

Ukichagua kujaribu kufanya usafi wa sikio nyumbani vijiti vya pamba si salama kuingiza kwenye mfereji wa sikio bali inaruhusiwa kusafishia eneo la nje pekee.

Hata hivyo, ili kuepusha ajali inashauriwa acha kabisa kutumia vijiti hivyo kuchokonoa sikio. Mtoto anaweza kuona akaiga akapata madhara. Badala yake, unaweza kutumia kitambaa kilichochovywa kwenye maji ya vuguvugu kufuta eneo la nje la sikio.

Unaweza pia kutumia dawa za matone kuweka matone sikioni na kulainisha nta, ambazo zimeruhusiwa hata bila kuandikiwa. Muhimu fuata maelekezo ya namna ya kutumia. Ukiacha matone, kuna namna nyingine kadhaa za kuweka sikioni dawa ya kulainisha nta ili itoke yenyewe.

Kulinda sikio

Ukiacha usafi, mambo mengine muhimu ya kufanya ili kulinda masikio yako ni pamoja na kutoingiza vitu vidogo kwenye masikio yako. Haupaswi kuweka kitu chochote kidogo ndani ya mfereji wa sikio kwa sababu kinaweza kusababisha jeraha kwenye mfereji au ngoma ya sikio. Punguza kukaa katika maeneo ya kelele, ikibidi vaa viziba masikioni. Pumzisha masikio yako kutumia vipokea sauti vyako (earphones, headphones). Ukituma weka sauti ya chini. Usipandishe sauti ya redio ya gari lako juu sana.

Kausha masikio yako baada ya kuogelea. Tumia kitambaa kufuta sehemu ya nje ya sikio, na uinamishe kichwa chako ili maji yoyote ya ziada yatoke. Ukiona mabadiliko yoyote ya usikivu yanayotokea baada ya matumizi ya dawa fulani, wasiliana na daktari.

جُمادى الأول

SAIKOLOJIA

MWANDISHI MAALUM

Zijue dalili kuwa unapitia manyanyaso ya kihisia

Unyanyasaji wa kihisia ni aina ya ukatili ambao mtu anatendewa kiasi cha kumsababishia maumivu kiakili/kihisia. Manyanyaso ya kihisia yanaweza kutokea katika mahali pa kazi, nyumbani katika familia au kwenye mahusiano ya ndoa.

Manyanyaso ya kihisia yanaweza kuwa hatari na yenye madhara kuliko manyanyaso ya kimwili kama kupigwa na kadhalika. Unyanyasaji wa kihisia unaweza kuwa wa wazi kama vile matusi kwa njia ya maneno au ishara yenye lengo la kudhalilisha, vitisho, maneno ya kufedhehesha na ya kudharau hadharani, kunyang'anywa watoto, kuingiliwa faragha, kutishiwa kuuawa, vitendo vya wivu wa kupindukia na kutishia kutoa siri.

Lakini, wakati mwingine unyanyasaji wa kihisia hauko wazi sana kiasi kwamba hata muathirika mwenyewe hajui kuwa anapitia unyanyasaji. Zipo dalili nne ambazo nitazitaja zinazoweza kukujulisha kama unanyanyaswa kihisia kisirisiri.

Dalili ya kwanza: Ukosoaji mara kwa mara na kutoona mema

Umewahi kukutana na watu ambao wao hawaoni jema lako lolote, bali chochote ufanyacho hutafuta namna ya kukosoa? Pengine anapokosoa hivyo, kuna mema mengi na makubwa uliyomfanyia au unaendelea kumfanyia. Hata hivyo, watu wa aina hiyo wamadhani wema wanaofanyiwa ni haki yao, hivyo hawaoni haja ya kushukuru na kuacha kunung'unika kwa makosa madogo.

Wanaume wanapitia sana mateso haya ya kihisia. Atahangaika kila siku kuhakikisha familia inakula, inatibiwa, watoto wanaenda shule lakini anapokea lawama na kuonekana hafanyi chochote kwa sababu kashindwa kumnunuia mke simu mpya!

Hata kazini, mambo ya aina hii hutokea: kuchukulia poa kazi ya mtu. Mtumishi pengine ni dereva tu lakini anajua na kusambaza bidhaa kwa wateja wa kampuni na hivyo kua mhimili katka mauzo. Lakini bosi haoni thamani hiyo ya mfanyakazi bali analalamkika makosa madogo. Mara nyingi wenye tabia hizi za unyanyasaji huishia kujuta!

Ukosoaji huu wa mara kwa mara unashusha hali ya mtu kujiamini na kujithamini, inapunguza morali ya kazi, na inaweza kusababisha sonona.

Dalili ya pili: Kukumbusha makosa

Dalili hii ya unyanyasaji wa kijinsia inahusu tabia ya mtu kukumbusha makosa yako ya nyuma mara kwa mara kukuteza nguvu au kuunganisha na ushahidi mpya wa mazingira kujenga hoja kuwa umefanya tena kosa.

Sababu ya kutumia kosa la zamani ni kukunyon'gonyesha ukose nguvu ya kujitetea. Ni kama kusema: "Kama ulifanya kipindi kile, na leo umefanya. Safari ile pia hukuwa unapokea simu na leo hupokei. Ni yaleyale." Ni unyanyasaji pia iwapo mtu anakuza makosa madogo.

Wengine, hasa kwenye mahusiano, hutumia hii kukushurutisha ukubaliane na jambo lake, hasa maombi ya pesa. Mwisho wa siku, unaweza kujikuta unatoa kipaumbele kwa shida zake kuliko za kwako kwa sababu unajisikia kama anakudai wema kwa sababu ya makosa uliyofanya. Hii inanyong'onyesha na kukupunguzia kujithamini.

Dalili ya tatu: Kutaka kukudhibiti

Namna nyingine mtu anaweza kukunyanyasa kihisia ni kwa kukudhibiti kila nyanja ya maisha yako. Moja ya mbinu za kukudhibiti ni kuzuia mahusiano yako na watu wengine au kukupangia nani uhusiane naye na usiongee naye. Pia, katika mbinu nyingine ni kukwambia nini cha kufanya na nini usifanye.

Wakati mwingine watataka kukudhibiti hata kwenye nini cha kufikiri. Mtu anakuuliza kwani unawaza nini, na usipomwambia anakupa neno la kukufanya ujisikie umemkosea wa kutomwambia. Utasikia: "Eeh najua huniamini... ingekuwa fulani ungeshasema."

Katika mbinu nyingine za kukudhibiti ni kukueleza namna ya kutumia muda wako na wangependa muda wako wote uutumie kwa kumshirikisha yeye. Pia, aghlabu watahalalisha tabia hiyo kwa kudai wanakupenda na kukujali. Hawaishii tu kukudhibiti, lakini pia watataka kukuelekeza namna ya kufanya kila kitu, hata vitu vidogo. "Nenda msalani, jisaidie, piga mswaki halafu uchukue wudhu uje uswali."

Madhara ya mtu kukudhibiti ni kukufanya uishi bila maingiliano na jamii yako wakiwemo ndugu, marafiki na majirani. Mwisho wa siku, myanyasaji anakufanya umtegemee yeye kwa kila kitu – jambp ambalo kiasili haliwezekani Unyanyasaji wa kihisia kwa mbinu ya kukudhibiti pia unazuia ukuaji wako kitaaluma na kikazi.

Dalili ya nne: Kutoheshimu mipaka

Umewahi kusumbuliwa na mambo ya kazi usiku wakati umepumzika na familia yako ilhali jambo lenyewe wala siyo la dharura? Wakati mwingine, mwenza analazimisha kujua masuala yako ya kazi, mengine yakiwa ni ya siri zinazogusa heshima za watu?

Katka maisha kuna mipaka ya uhuru wa mtu lazima iheshimiwe. Sawa, mtu anaweza kuwa muajiriwa wako lakini pia ana maisha binafsi anayoyaishi nje ya kazi. Mtu ana mke, ana watoto, ana wazazi, ana imani ya dini na kadhalika. Pia, ana harakati zake za binafsi za kujitafutia riziki zaidi. Mpaka wa muda wa majukumu yake ya kazi na muda wa mambo binafsi lazima uheshimiwe.

Dalili ya tano: Kukosoa na kupuuza hisia zako

Kukosoa hisia za mtu mara kwa mara ni dalili nyingine ya manyanyaso ya kihisia. Hii hutokea pale mtu anapodharau hisia zako - hasa unapokasirika - na kuonesha kwamba hazistahili katika jambo husika. Utawasikia wakosoaji hao wa hisia za watu wakimwambia mtu: Acha jazba, usichukulie kibinafsi, hili nalo ni jambo la kukasirika? Una hasira za haraka sana, acha gubu na kadhalika.

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

/islamicftz

NA MUSSA IMANI SHEHA

Mapenzi ya kweli ni mlezi wa familia

Qur'an imetunukulia tukio zito linatuonesha jinsi mtu anavyoweza kuathirika na mapenzi yasiyofuata nidhamu, yakamfedhehesha na kumtia aibuni. Hilo ni tukio la mke wa waziri mkuu wa Misri wa zama hizo kutokea kumpenda mfanyakazi wake, Yusuf, Nabii wa Mwenyezi Mungu (amani ya Allah iwe juu yake).

SEHEMU YA TATU

Mapenzi kwa kijana wake yaliumiliki moyo wake, yakamzingua na kumsahaulisha nafasi yake kama mke wa mheshimiwa. Mwishowe alipituka miiko ya ndoa baada ya kumtaka Nabii Yusuf kimapenzi.

Mapenzi yaliivuruga akili ya Zuleikha hadi akawa hoi. Katika kumtaka kimapenzi, kwanza, alitumia mbinu za ushawishi wa kike na ulaghai, na kisha akatumia nguvu na mabavu katika kulazimisha mapenzi batili na hatimaye yakamdhalilisha!

Tukirejea Qur'an, Mwenyezi Mungu anasema: "Na (mwanamke) ambaye (Yusuf) alikuwa nyumbani mwake alimtamani (Yusuf) kinyume na ridhaa yake, na akafunga milango akamwambia, 'Njoo.' Yusuf akasema, 'Najikinga kwa Mwenyezi Mungu (kufanya zinaa) hakika (mumeo) ni bwana wangu, ametengeneza vyema makazi yangu (nyumbani mwake, siwezi kumfanyia hiyana).' Hakika madhalimu hawatengenekewi." [Qur'an, 12:23].

Qur'an inatufahamisha kwamba, akiwa ameshamuingiza katika chumba cha siri alalako na mumewe, mwanamke aliazimia kisawasawa kumlazimisha Yusuf. Alikusudia afanikishe hata kwa kumpiga.

Yusuf naye alijizatiti na kuamua kukimbia. Hali iliyopelekea kumchania kanzu yake mgongoni, katika za kumshika kwa nguvu na kutaka kumrudisha chumbani!

Wanawake wenzake wamshangaa

Fedheha iliyomfika Zuleikha mitaani haikadiriki. Watu, hususan wanawake wenzake, walimsema vibaya. Qur'an inasema: "Wanawake wa mji ule wakasema, '(Jamani) mke wa waziri anakwenda kumtamani mtumishi wake pasina yeye kutamaniwa! Hakika amemuathiri sana kwa mapenzi, bila shaka sisi tunamuona (mke wa waziri) yumo katika upotofu (kosa) la Dhahiri)'" [Qur'an, 12:30].

Lawama zilipozidi, mke wa waziri, alijitoa kimasomaso kwa kutaka kuwaonesha kilichouteka moyo wake ili waelewe kwamba hafai kulaumiwa aliyechanganyikiwa kwa kumpenda Yusuf. Pia, alitaka atazame, je wao wataweza kumiliki nyoyo zao?

"Basi aliposikia maneno (lawama) zao, aliwaita na kuwaandalia karamu, na akampa kila mmoja wao kisu (cha kukatia vifaa) na akamwambia (Yusuf) jitokeze mbele yao. Basi, walipomuona waliona ni kitu kikubwa kabisa na wakakata mikono yao (wakiwa wameshughulika kumtazama Yusuf). Wakasema, 'Haashalillah! Huyu si mwanadamu, hakuwa huyu ila ni malaika mtukufu." [Qur'an, 12:31].

Madhara yake

Katika kisa hiki ambacho Allah amekiita "ahsanal-qasas" (kisa kizuri zaidi), tunaona madhara ya mapenzi yasiyofuata muongozo wa Allah yamejitokeza katika maeneo kadhaa.

Eneo la kwanza ni ile kuleta aibu katika nyumba ya mheshimiwa waziri, na vilevile fedheha iliyomkuta Zuleikha pamoja na mume (waziri) wenyewe. Na kama si udhaifu wa wadudu wa wivu katika moyo wa mume huyo, tungelisema hata usalama wa ndoa nao ungelikuwa hatarini.

Eneo la pili ambapo madhara yanaonekana ni dhulma ya kutiwa hatiani mtu asiyehusika, akaishia kubaki gerezani miaka kadhaa bila ya kosa, kama aya zilivyoendelea kusimulia.

Ndiyo maana katika mfululizo wa makala yetu tumesema kuwa mapenzi yasipojengwa juu ya misingi ya kumcha Mwenyezi Mungu na kuwa ya kishikaji tu, hatima yake ni kuwaangamiza wapenzi na kuwaondolea heshima zao. Mpaka leo tunashuhudia matukio kama haya.

Kwa sababu ya mapenzi yaliyo kinyume na misingi sahihi, watu hutwangana ngumi klabuni, ndoa huvunjika, wengine hufukuzwa kazi, baadhi huharibu mitaji yao, kuna wanaowatelekeza wake na watoto wao na wanaovunja urafiki wao nk. Yote hayo kwa sababu ya mapenzi kuwekwa mahala sipo yakakosa kuchunga mipaka yaliyowekewa na Muumba.

Mapenzi baina ya wanandoa

Naam, hapa kwenye ndoa ndiyo shamba pekee halali linalofaa kupandikiza mche wa mahusiano ya kijinsi baina ya wakubwa wawili.

Awali ya yote, tujue kwamba hili ni jambo la kimaumbile sana. Siku zote moyo wa mwanamume humili (huvutika) kwa mkewe na huliwazika wanapokuwa pamoja, kama ambavyo mke naye hujisikia faraja (burdani) anapokuwa pamoja na mumewe.

Hayo tunajifunza katika aya ifuatayo: "Na katika dalili zake ni kukuumbieni kutokana na jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya zimo ishara kwa watu wanaofikiri." [Qur'an, 30:21].

Wanandoa wana jukumu kubwa la kuelewa nafasi na umuhimu wa mapenzi katika ndoa yao, na kuelewa kwamba mapenzi ndiyo chachu ya ustawi wa hata familia. Kadhalika, wanapaswa kufanya juhudi za pamoja katika kulistawisha penzi na kulitunza ndani ya nyumba yao ya ndoa.

Kwa hali hiyo, wanandoa pia hawana budi kujifunza na kujua vichocheo vinavyoweza kufanya mapenzi yao ya kindoa kuwa mabichi, yasiyonyauka, ambapo msingi mkuu wa kufikia hayo ni wawili hao kutekeleza haki na majukumu kisharia.

Faida za wanandoa kupendana

Kabla ya kudadavua vikuza mapenzi katika ndoa ya Waislamu, tunapenda kumtajia msomaji wetu mpendwa kwa ufupi faida zinazopatikana katika ndoa yenye mapenzi.

Mosi, kuishi kihisia: Hisia za mke huwa pamoja na hisia za mume, na kupelekea kuwa na furaha siku zote. Hali hiyo humfanya kila mmoja kuridhika na hali yoyote atakayokuwa nayo mwenza wake.

Mbili, kuhurumiana: Kuhurumiana, maana yake, ni ile hali ambapo mmoja anapopata tatizo yule mweza wake anahisi ni la kwake. Hali hiyo huzaa sifa ya ukarimu.

Faida ya tatu ni ulinzi kwani kutokana na kupendana, kushikamana, kushibana basi yoyote kati ya wenza nukasirika pale mwenzake anaposemwa vibaya au kwa kutokea mwingine akataka kulichezea penzi lao.

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

جُمادى الأول

/islamicftz

MAKALA

NA SAID RAJAB

SEHEMU YA NNE

Kwanini Wapalestina wana ujasiri mkubwa?

Katika makala iliyopita tulimalizia na visa vya Har'aam na Khabbab, ambavyo vinaonesha jinsi imani inavyoweza kumfanya mtu kuwa madhubuti hata akipatwa na mtihani wa aina gani, kama tunavyoshuhudia hivi sasa huko Gaza.

Tulisema, watu wengi katika nchi za Magharibi wamekuwa wakiingia kwenye Uislamu kutokana na kushangazwa na ujasiri na umadhubuti wa watu wa Gaza, mambo ambayo yamechochea watu wengi kuukubali Uislamu. Sasa endelea na sehemu inayofuata...

Kuanguka kwa haki za binadamu

Vita ya Gaza imewafichua watu wengi wa Magharibi ambao wamekiri kwamba maadili yanayopigiwa debe ya haki za binadamu na uhuru vimekuwa ni vielelezo tu vinavyofunika ubabe, dhuluma na utawala wa kikoloni.

Kelele za demokrasia na haki za binadamu zinatumika kwa kuchagua na kupuuzwa kabisa pale zinapokinzana na maslahi ya nchi za Magharibi, hususani kuhusu Palestina. Kuikataa kwao kadhia ya Palestina, licha ya kujua ukweli wa dhuluma inayofanywa ukanda wa Gaza, kunachochewa na kudumisha hali iliyopo ya mienendo ya dhuluma duniani.

Vita ya Gaza imewaibua watu wengi katika nchi za Magharibi ambao wanaamini katika maadili ya haki za binadamu na usawa. Kwa muda mrefu waliyachukulia maadili haya kama msingi wa jamii zao na wakaazimia kuyachukua kama msingi wa ubora wa maadili na ustaarabu.

Hata hivyo, mauaji haya ya kimbari yanayoendelea huko Gaza yamewakatisha tamaa wafuasi wa haki za binadamu na wamepuuza maadili hayo. Vita ya Gaza imethibitisha uongo wa kauli za 'haki' za binadamu. Hili limewaacha hoi Wamagharibi wenye nia njema wakiwa wamekata tamaa kabisa, wakishushwa na yale waliyokuwa wakiyaabudu na kuyaamini kwa dhati badala ya Muumba wa mbingu na ardhi.

Lakini, mapenzi yao ya haki yameendelea kuwa na nguvu, na ndiyo maana wamewageukia mashujaa wa Gaza wanaopigania ukweli na haki ili kupata kile walichokipoteza. Walitamani kuwa kama wao baada ya kuona mifumo na viongozi wao wamewaangusha, na wakagundua kwamba watu wa Gaza wanamuabudu Mungu Mlezi wa mbingu na ardhi, basi Allah 'Azza wa Jallah' akawaongoza kwenye Uislamu.

Mwisho wa vikwazo vya makureish

Wakati wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie), mmoja wa viongozi wa kabila la kikureish aitwae Mut'im ibn 'Adi aliingilia kati mgogoro uliokuwepo kati ya makureish na Waislamu wa Makka ili hatimae kukomesha vikwazo vya miaka mitatu vilivyowekwa na makureish dhidi ya Waislamu.

Baadaye Mut'im alimpa ulinzi Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) baada ya kupigwa mawe na kujeruhiwa vibaya katika mji wa Twaif. Mtume alikuwa akikumbuka nia njema ya Mut'im baada ya vita vya Badr, ambapo Maswahaba walikuwa wamewashikilia mateka wa vita.

Mtume alisisitiza kuwa angewaachia huru mateka kwa ajili ya Mut'im iwapo angekuwa hai, kama alivyosimulia Jubayr (mtoto wa Mut'im) ambaye wakati huo alikuwa ameshaukubali Uislamu, [Bukhari kutoka kwa Jubayr Ibn Mut'im].

Wako wapi leo akina Mut'im, ambao kwa sababu yao mateka wa Israel wangeweza kuachiwa huru na kuondoa mzingiro wa Gaza?

Dhana mpya ya upinzani na uthabiti bila nyenzo

Katika simulizi nyingi za kisasa za Nabii Daudi dhidi ya Goliath, iwe ni eneo gumu la Afghanistan, kutokuwa na usaidizi kutokana na mashambulizi ya anga, uvamizi wa Marekani wa Ghuba mwaka 1961, au kujiondoa kwake kutoka Vietnam kwa sababu ya mbinu za msituni, watu duni mara nyingi hupewa sifa ya aina fulani kwa manufaa ya kimkakati au kijeshi.

Mandhari, usaidizi kutoka nje, au uwezo wa kisiasa, kwa kawaida huelezea mafanikio yasiyowezekana. Lakini Gaza ipo kinyume kabisa na utaratibu huo, kwani hakuna milima ya kuikinga, hakuna usaidizi kutokana na mashambulizi ya anga, hakuna ushirikina wa kisiasa na hata mahitaji muhimu ya binadamu kama vile chakula, maji na umeme!

جُمَادَى الأُوْل

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

ZAHARANI BARAKA

Usimwambie mtu siri mliyowekeana na Muawiyah

Anas bin Malik (Allah amridhie) amesema: “Siku moja Mtume (rehema na amani zimshukie) alinijia wakati nikicheza pamoja na watoto wenzangu, akatusalimia kisha akanituma kufanya jambo fulani, hivyo nikachelewa kurudi nyumbani kwa mama yangu.”

Niliporejea mama aliniuliza: “Kitu gani kimekuchelewesha?” Nikamwambia: “Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa na jambo fulani akanituma.” Mama akaniuliza: “Ni jambo gani hilo.” Nikamwambia: “Hakika hiyo ni siri kati yangu na Mtume.” Mama akaniambia: “Basi usimsimulie yeyote siri ya Mtume (rehema na amani zimshukie).”

Baada ya siku nyingi kupita, Anas aliombwa na mmoja wa marafiki zake amtajie ile siri baina yake na Mtume, Anas akamwambia: “Naapa kwa Allah, laiti ningekuwa nimemsimulia mtu yeyote, basi hata wewe ningekusimulia.” **[Muslim]**

Tunayojifunza kutokana na tukio hili

Mtume (rehema na amani zimshukie) aliilea familia yake katika tabia hii nzuri, kama ilivyothibiti katika simulizi ya mama Aisha (Allah amuwie radhi) ambaye amesema: “Wakati mmoja Fatima (Allah amridhie) alikuja (nyumbani kwangu), na mwendo wake ulikuwa unafanana sana na mwendo wa Mtume (rehema na amani zimshukie).” Mtume akasema: “Karibu ewe binti yangu.”

Mtume alimkalisha Fatima upande wake wa kulia kisha akamnong’oneza jambo, mara Fatima akaanza kulia.” Nikamuuliza: “Unalia nini?” Mtume akazungumza tena na Fatima kwa siri, Fatima akacheka, nikamwambia: “Sijapata kukuona ukiwa na furaha inayokaribiana na huzuni kama uliyokuwa nayo leo.”

Kisha nikamuuliza kuhusu alichokisema Mtume (rehema na amani zimshukie), nae akaniambia: “Sijawahi kuvujisha siri ya Mtume (rehema na amani zimshukie).” Hivyo Fatima akaendelea kuitunza siri ile.

Siku chache baada ya Mtume kufariki nilimuuliza tena kuhusu siri yake na Mtume, akasema: “Mtume alininong’oneza kuwa Jibril alikuwa na kawaida ya kuja kumsomesha Qur’an kila mwaka mara moja, lakini mwaka huu amefanya hivyo mara mbili. (Kwa hiyo) sioni sababu ya kufanya hivyo kwani ajali yangu (kifo) imekaribia, na wewe utakuwa wa kwanza katika familia yangu kuungana nami, ndipo nikalia, nae akaniambia, ‘Kwani wewe huridhii kuwa bibi (mkuu) wa wanawake wote Peponi?’ Basi nikacheka kwa sababu hiyo.’” [Bukhari].

Tukio hili la Anas bin Malik (Allah amridhie) ni moja kati ya matukio mengi yanayoonesha namna wazazi katika zama za Mtume (rehema na amani zimshukie) walivyoshughulika na suala la maadili na tabia njema kwa kuhakikisha wanawalea watoto wao katika misingi hiyo.

Mtume alimpa Anas jukumu la kutunza siri yake licha ya umri wake kuwa mdogo. Mama yake alipogundua kuwa jambo alilotumwa na Mtume kulishughulikia ni la siri baina yake na Mtume alimsisitiza aifiche siri hiyo na akamuusia asiifichue kwa mtu yeyote.

Hii ni ishara njema kwamba watoto wanaweza kubeba majukumu makubwa tangu utotoni mwao, wanaweza kuaminika katika yale yaliyopo katika uwezo wao ikiwa watalelewa katika misingi ya tabia njema na maadili ya Kiislamu.

Anas mwenyewe anasema: “Mtume (rehema na amani zimshukie) alinipa siri, nami sikufichua siri hiyo kwa yeyote baada yake, na hata mama yangu aliponiuliza sikumwambia.” Ibn Hajar (Allah amrehemu) amesema kuhusiana na kauli hii ya Anas: “Ni kama vile siri hii inahusiana na wake wa Mtume (rehema na amani zimshukie). Ingekuwa suala hili linafungamana na elimu, basi isingefaa kwa Anas kuficha siri hiyo.”

Hudhayfah apewa lakabu ya ‘msiri wa Mtume’

Hudhayfah Ibn al–Yaman (Allah amridhie) ni miongoni mwa Maswahaba waliopewa majina ya utani (lakabu) kutokana na mambo waliyokuwa wakifanya. Siku moja Mtume (rehema na amani zimshukie) alimtajia Hudhayfah majina ya wanafiki waliokuwepo katika zama zake, lakini Hudhayfah alificha siri hiyo kwa muda mrefu na hakuwa tayari kumtajia mtu yeyote jina au majina ya wanafiki aliyotajiwa na Mtume.

Kutokana na sifa yake hii watu wakampa jina la utani la ‘msiri wa Mtume’. Khaythama (Allah amrehemu) amesema, alifika kwenye mji wa Madina akamuomba Allah amfanyie wepesi apate rafiki mwema, Allah akamfanyia wepesi akawa pamoja na Abu Huraira (Allah amridhie). Abu Huraira akamuuliza: “Umetokea wapi?” Khaythama akamjibu: “Nimetokea mji wa Kufah (Iraq) na nimekuja (Madina) kutafuta kheri.”

Abu Huraira akamuuliza: “Kwani nyinyi watu wa mji wa Kufah miongoni mwenu si yupo Sa’ad Ibn Abi Waqqas ambaye dua zake hukubaliwa (Mustajaabud–da’awa), Ibn Mas’ud ambaye alikuwa akimuandalia Mtume maji ya udhu pamoja na viatu vyake, na Hudhayfah bin al–Yaman ambaye alikuwa msiri wake?” [Imepokewa na Tirmidhi].

Abu Huraira alimtajia Khaythama baadhi ya majina ya Maswahaba yanayotokana na sifa bora walizokuwa nazo. Ni uzuri ulioje pale jina la utani na maarufu linapotokana na tabia njema na uaminifu wako.

Salaf waliwalea watoto wao katika msingi huu

Siku moja Muawiyah bin Abi Sufyan (Allah awaridhie) alifanya mazungumzo ya siri na Walid Ibn Utbah, baadae Walid akamwambia baba yake: “Hakika leo nilikuwa na mazungumzo ya siri na Amiirul Muuminina, nami sioni kama anaweza kukuficha jambo ambalo atamweleza mtu mwingine.”

Walid alikusudia kumwambia baba yake siri hiyo, baba yake akamwambia: “Usimsimulie yeyote siri mliyowekeana na Amiirul Muuminina kwani kuficha siri yake ni bora kwako.”

Wazazi kuweni mfano wa kuigwa katika kutunza siri

Wenye hekima walisema: “Hakika watu waaminifu katika kutunza siri ni wachache sana kuliko waaminifu wa mali, na kuhifadhi mali ni rahisi sana kuliko kuhifadhi siri kwa sababu, hazina ya mali hufungwa kwa milango na kufuli madhubuti, wakati hazina ya siri ipo wazi na husambazwa kwa ulimi. Na katika maajabu ni kwamba kadri mali inavyoongezeka hudhibitiwa na kulindwa kwa umakini mkubwa, lakini siri zinapokuwa nyingi huwa katika hatari ya kupotezwa na kusambazwa.

Na siri zipo aina nyingi; kuna siri baina ya marafiki, siri baina ya wazazi na watoto, na siri kati ya walimu na wanafunzi. Miongoni mwa siri nzito ambazo Uislamu umetilia mkazo zitunzwe na kuhifadhiwa ipasavyo ni mambo wanayofanya wanandoa (mume na mke).

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: “Hakika miongoni mwa watu waovu kabisa mbele ya Allah Siku ya Kiyama ni mtu aliyejamiiana na mkewe, na mke aliyestarehe na mumewe kisha mmoja wao akatangaza siri hiyo.” [Muslim]. Hii ina maana kuwa ni haramu kusimulia mambo ya ndoa hadharani au hata kwa rafiki wa karibu.

جُمادى الأول

MAKALA

SEHEMU YA TATU

Asia bint Muzaahim: mwanamke shujaa wa Imani

Tunayojifunza kutokana na kisa chake

Baada ya kupata muhtsari wa kisa cha bi Asia (amani ya Allah iwe juu yake) katika matoleo mawili yaliyopita, leo tuaangalia mafunzo muhimu tunayoyapata kutokana na kisa hiki cha mmoja wa wanawake bora kabisa tangu Allah Mtukufu alipomuumba mwanadamu.

Moja ya mafunzo makubwa ni kuwa, ukatili wa waume hauishii kwa watu wa kando; mtu anaweza kumkatili mke wake na kumnyanyasa. Kwa hiyo haya tunayoyashuhudia na kuyasikia leo hii ni mwendelezo wa udhalilishaji waliouanzisha waume makatili kama Fira-un kwa wake au wanawake wao.



Asia bint Muzahim alikuwa mwanamke mwema na hakuwa na kosa lililomtia hatiani kiasi cha kustahili kuteswa vikali. Pengine, kosa lake, ambalo kiuhalisia sio kosa, ni kuwa na imani juu ya Mola wake, Mola wa haki ambaye pekee anastahili kuabudiwa.

Tunaona kuwa uovu na ukatili huzitawala busara za baadhi ya waume, kisha wakawafanyia unyama wake zao bila ya kujali. Qur'an inawaasa waume hao: "Na kaeni nao (wake zenu) kwa wema na kama mtawachukia (basi msiwaache) kwani huenda mkakichukia kitu na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake." [Qur'an, 4:19].

Na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Muumini mwanamume asimchukie muumini (mwenzake) mwanamke, akichukia tabia yake moja ataridhia tabia yake nyingine." [Muslim]. Kwa hiyo, Uislamu unakemea vikali tabia ya kunyanyasa wanawake na watoto pia.

Aidha, Uislamu unawaasa sana wanaume wasio na shukran, wayafumbiao macho mambo mema, mapenzi na huduma wanazofanyiwa na wake zao na badala yake wakawalipa kejeli, dharau, matusi na vipigo Uislamu si dini inayoruhusu udhalilishaji wa aina yoyote, ukiwemo kuwavunjia watu heshima zao na kuwapiga bali Uislamu unaita watu kwenye usawa, uadilifu, kuwahurumia na kuwaheshimu wanawake pamoja na kusamehe udhaifu wao.

Na ile aya iliyokuja kuwaruhusu waume kuwaadabisha wake manashiza (watukutu) kwa kuwapiga, inatakiwa tuipe mazingatio. Kwanza ijulikane kuwa wanaoruhusiwa kupigwa ni wanawake watovu wa adabu; na pili, iwe baada ya kuchukua hatua za kuwaonya na kuwahama vitandani. Tatu, utekelezaji wa hatua hii ya tatu (kipigo) uwe kwa uangalifu wa kutosha. Kipigo kisiwe cha kuvunja viungo au kuchubua ngozi na kuvujisha damu.

Allah Mtukufu anasema: "...na wanawake ambao mnaona uasi wao kwenu waonyeni na waacheni peke yao vitandani na wapigeni. Na kama watakutiini msiwatafutie njia (ya kuwaudhi) hakika, Mwenyezi Mungu ndie wa juu mkuu." [Qur'an, 4:34].

Turejee hadith ya Abdillah bin Zam-at aliyesema kuwa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) katika moja ya khutba zake aliwaasa waume wawafanyie wema wanawake zao. Kisha akasema: "Hivi mmoja wenu anaweza kumpiga mke wake kipigo cha mtumwa kisha akalala naye (akamtaka unyumba) siku ile ile!?" Maswahaba walipocheka akawaambia: "Yaani mmoja wenu anachekelea uovu anaoufanya!" [Bukhari na Muslim].

Mazingatio

Kutokana na nususi tulizozirejeea tunajifunza mambo muhimu yafuatayo: Moja, sharia ya kipigo haimuhusu mwanamke mtiifu aliyekosea kibinadamu tu. Pili, mwanamke hapigwi kabla ya kuonywa na kuhamwa kitandani.

Tatu, aliyeacha ununda baada ya hatua za awali za kuadabishwa, kipigo hakimuhusu bali mume anatakiwa aachane na yaliyopita na maisha yaendelee kwani hakuna binadamu asiyekosea.

Nne, wanaume wajisikie aibu mmoja wao kumpiga mkewe kisha akamuomba unyumba mkewe huyohuyo na pengine mara tu baada ya kipigo, kwani hilo haliendani na ubinadamu.

Wanaume waache kuwanyanyasa na kuwadhalilisha wake zao kwani hizo ni tabia za kifirauni.

Funzo jingine tunalolipata kutokana na simulizi ya Asia ni ile tulioitaja katika toleo la wiki ya jana kwamba, siri ya Allah katika uendeshaji wa mambo yake ni kubwa na hakuna anayeijua ila Yeye.

" Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha." [Qur'an, 6:59].

Watu wa nyumba ya Fir-aun pamoja na yeye mwenyewe hawakujua wala hata kutazamia kwamba, itatokea Musa kuwa mtume na mwana harakati ambaye atauangusha utawala uliodumu kwa muda mrefu wa Mafarao wa Misri. Basi alipangalo Allah lazima litimie.

Simulizi inatufunza tena ujabari wa viongozi madhalimu waliolewa madaraka na jinsi wanavyokuwa na hofu ya tawala zao kuangushwa. Wako tayari hata kupoteza uhai wa wengine katika juhudi za kuhakikisha wanabaki na kudumu.

Angalia jitihada alizozifanya Fir-aun katika kulinda utawala wake baada ya kutishiwa. Alipitisha sharia ya kupoteza uhai wa watoto wa Wana wa Israil tena kwa muda mrefu bila ya hata hisia ya utu na ubinadamu.

Wanawake na subira katika maisha ya ndoa

Wanawake waliojaribiwa na Mola wao kwa kuolewa na wanaume waovu wanyanyasaji, wanatakiwa wajifunze subira kupitia kisa cha mwanamke huyu ilii kuchunga maslahi yanayopatikana katika ndoa zao.

Hakuna mwanamke aliyewahi kuishi katika mtihani mkubwa zaidi katika ndoa kuliko bi Asia. Alivumilia machungu na maudhi ya mumewe jabari aliyejiita mungu mkuu hadi akaondoka duniani kwa mateso lakini akiwa ni mwenye kuridhiwa na kurehemewa na Mola wake.

Tunamuomba Allah atusamehe waja wake na aturehemu, amin.

Kwa mrejesho, wasiliana na mwandishi kwa namba 0773181494

IMAAN
Jumapili Novemba 3, 2024

جُمادى الأول

/islamicftz

FAHAMU USIYOYAJUA

NA ABDILLAHI MASHI

KING KOBRA:

Nyoka pekee anayelinda mayai yake

Allah Aliyetukuka ndiye aliyeumba ulimwengu na viumbe vyote bila usaidizi wa yeyote, na Yeye ndiye anayeuendesha ulimwengu huu. Kwa hivyo, Yeye ndiye anayestahiki kuabudiwa kwa sababu hakuna yeyote aliyemsaidia katika uumbaji. Kuna viumbe wengi ulimwenguni tunaowafahamu na tusiyowafahamu, na kila uchao wavumbuzi wanaleta taarifa ya uvumbuzi wa viumbe wapya. Katika safu hii, leo acha tukaone ukubwa wa Allah kwa kumtazama nyoka aitwae 'King kobra.'

Huyu ni nyoka mwenye ngozi nzito kiasi kutoka familia ya 'elapidae'. Wataalamu wa elimu ya viumbe hai wanasema, kuna zaidi ya aina 200 za kobra, wakiwemo Indian kobra, Egyptian kobra, Cape kobra, blacknecked spitting cobra , monocled kobra, na huyu king kobra ambaye ndiye mkubwa zaidi.

King kobra wanapatikana barani Asia tu, huwezi kuwakuta Amerika, Ulaya wala Afrika. Katika bara la Asia, king kobra wanapatikana kwa wingi nchini India, Myanmar, Vetnam, Thailand na sehemu za Kusini mwa Asia.King kobra hupendelea kujificha kwenye mapori makubwa na hawapendi kumshambulia mtu. Asilimia kubwa ya watu wanaong'atwa na nyoka hawa ni wale wenye tabia ya kucheza nao.

Miongoni mwa nyoka wenye sumu kali, huyu ndiye mkubwa kuliko wote. Nyoka huyu anaweza kufikia urefu wa kati ya futi 18.5 hadi 18.8 sawa na mita 5.6 hadi 5.8. Madume ya nyoka hawa ni wakubwa kuliko majike, tofauti na nyoka wengine. Nyoka wengi, majike huwa ni wakubwa kuliko madume.

Kule Asia, hasa katika nchi za India na Sri Lanka, king kobra na baadhi ya nyoka wengine, ni alama kubwa katika dini za kibudha na kihindu, ambazo Uislamu unazitazama kama dini potofu na za kishirikina. Uislamu unamtazama king kobra na nyoka wengine kama viumbe wengine na hawana utukufu wowote ule.

Tabia na sifa zao

Sifa mojawapo ya king kobra ni kwamba ana uwezo wa kuinuka theluthi ya mwili wake. Pia, anaweza kukugonga kisha akatulia hapo hapo, ila jua kuwa akifanya hivyo huwa anaacha sumu nyingi zaidi.Ijulikane pia kuwa king kobra ni nyoka asiye na hasira na ndiyo maana anatumiwa sana katika michezo ya kucheza na nyoka. Lakini ieleweke kuwa, vifo vinavyotokana na nyoka hawa ni vichache mno ukilinganisha na vifo vya ajali au watu wanaouawa na majambazi. Nchini India na Sri Lanka nyoka hawa wanatukuzwa sana, wana hadhi ya juu na hawauliwi.

Uzazi na chakula

King kobra hutaga mayai yake kwa nje (Oviparous). Nyoka huyu hutaga mayai kati ya 20 hadi 40 kisha huyatumbukiza kwenye majani yaliyopo kwenye kiota ili yapate joto, na hubaki hapo mpaka atotoe mayai yake.

Kwa upande wa chakula, king kobra anakula panya, ndege, mijusi, mayai na mamalia wengine wadogo. Licha ya kuwa na sumu kali, king kobra hana ujanja anapokutana na mnyama anayeitwa nguchiro.

Maajabu nane ya king kobra

Kwanza, king kobra ndiyo nyoka pekee anayelinda mayai yake, jambo ambalo huwezi kulikuta kwa nyoka wengine.

Pili, king kobra anapata hisia kwa kutumia ulimi wake kwani Allah, Mbora wa Uumbaji hakumjaalia kuwa na pua. Kwa maana hiyo, huvuta harufu kwa kutumia ulimi.

Tatu, king kobra amejaaliwa uwezo wa kuona mbali. Wataalamu wanatueleza kuwa nyoka huyu ana uwezo wa kuona hadi umbali wa mita 100, sawa na urefu wa kiwanja cha mpira.

Nne, nyoka huyu hana masikio, yeye hupata hisia kupitia ngozi iliyo chini ya mwili wake (earth born vibration).

Tano, inapotokea amemgonga kiumbe anayetaka kumla, basi huanza kumla kabla hata hajafa (hapendi kula mizoga). Hata hivyo, hii pia ni kawaida ya nyoka wengi.

Sita, nyoka huyu hutumia muda mfupi sana kumla kiumbe, na hamtafuni bali hummeza mzima mzima.

Saba, king kobra anawinda wakati wa mchana na mara chache usiku. Nchini Ugiriki, nyoka anayewinda mchana huitwa nyoka mla nyoka.

Nane, licha ya hatari aliyokuwa nayo, king kobra akikutana na binadamu hukimbia, lakini ukimchokoza anakuwa mkali na mkorofi.

Jinsi ya kujilinda na nyoka huyu

Wataalamu wanatuambia, unapokutana na king kobra, njia mojawapo ya kujilinda asikudhuru ni, kwanza rudi nyuma kisha vua shati lako au kofia umtupie chini. Baada ya hapo yeye huwa rahisi kushughulishwa na kile alichotupiwa kuliko wewe.